



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# NJIA TATU

LEo tutachukua somo la "njia tatu" ndani ya biblia. Kwa kawaida, tumesikia juu ya "njia mbili" lakini njia hii ya tatu ni ipi, unaweza kuwa unajiuliza? Leo mwishoni wa somo tutaona na kuelewa njia hiyo ya tatu pia!

Kwanza na tuchunguze njia mbili za kwanza tunazozijua, kama tunavyosoma sasa kutoka: mathayo[1] 7:13,14 – *"ingieni kupitia **mlango mwembamba**, kwa maana **lango ni pana na njia ni pana** ielekeayo katika **uangamivu**, nao ni wengi waingiao kwalo. Bali **mlango ni mwembamba na njia ni finyu** ielekeayo katika **uzima**, nao ni wachache wauonao"*

Yesu hapa anazungumza juu ya njia iliyopana yenye...... Lango pana "iendayo katika uangamivu, nao wapo wengi waingiao kwalo" na njia finyu yenye mlango mwembamba "iendayo uzimani, nao ni wachache wauonao"

Njia hizi mbili ni zipi? Kimapokeo zinafikiriwa kuwa zinaelekea mbinguni na kuzimuni! Je, ndio hivyo? Haya ni maneno yaliyosemwa na yesu, kumbuka!

Sasa na tusome jambo fulani kuhusu jinsi yesu anazungumza, katika mathayo 13:34 *"…..wala pasipo fumbo hakusemea nao"*

Yatupasa kukumbuka kuwa yesu daima alinena kwa mafumbo..! Pamoja na kunena kwake mafumbo 39 au hadithi ndogo ndogo pia

alizungumza kauli nyingine za kimafumbo. Kwa hivyo, hapa pia "njia" ni lugha za mafumbo znazotumika. Zina maana gani? Tunaweza kuielewa kwa mfano na kielelezo. Wakati mvulana mdogo au msichana anapojihusisha na vitendo visivyofaa na kuwa mpotovu wazazi wangemwita na kumuuliza hivi - "maisha yako yanakwenda katika njia ipi?" hii ina maana gani? Inarejelea namna ya maisha iliyochaguliwa! Yesu pia hapa anarejelea machaguo mawili ya namna za maisha zilizokuwepo katika siku zake - njia pana na njia finyu!

Pia, lazima izingatiwe kuwa hakuna hatima kama mbingu au kuzimu iliyotajwa. Moja, tunasoma inaelekea katika "uangamivu" na nyingine inaelekea katika "uzima". Hii ina maana gani? Ni nini maana ya "uangamivu" huu, na "uzima" huu? Lazima tujifunze njia hizi kwa undani ili kupata majibu!

**Njia ya kwanza - njia pana**

Hebu sasa tujifunze njia pana tunaposoma kutoka katika mathayo 7:13 *"ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana lango ni pana, na njia ni pana iendayo katika uangamivu, nao ni wengi waingiao kwalo"* nini kinamaanishwa kwa hii "njia pana"? Na nini maana ya - "uangamivu"? Tunasoma pia kwamba "wengi ... Wanaingia humo" hii ndiyo njia ambayo watu wengi wa ulimwengu wanatembea humo, inavyoonekana!! Njia hii ni ipi? Tunasoma kuhusu njia hii tena katika maandiko, katika mithali 14:12 *"iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti."*

Namna ya maisha au njia ya ulimwengu wa wanadamu "inaonekana kuwa sawa" kwao kwa sasa lakini mwisho wake tunasoma ni "njia za mauti." Ni "njia" ya aina gani ambayo inaishia "katika njia za mauti"? Jibu liko wazi katika biblia tunaposoma sasa kutoka katika warumi

6:23 *“…. Mshahara wa dhambi ni mauti…”* tunajua kwamba mauti ni tunda au matokeo ya dhambi. Hivyo "njia" hii lazima iwe njia ya dhambi! Na mauti ni uangamivu unaotajwa hapa! Fikiria tu!

Katika ulimwengu na maisha yetu, tunaona uangamivu(uangamivu) mwingi unaotuzunguka - uangamivu wa biashara kupitia hasara/kufilisika. Uangamivu wa nyumba au jengo - kwa moto au maafa ya asili. Uangamivu wa urafiki - kupitia ugomvi, wivu n.k. uangamivu wa miji/nchi - kupitia majanga kama vile tsunami, vita, matetemeko ya ardhi, vimbunga n.k. uangamivu wa ndoa - kwa talaka, uzinzi, n.k. uangamivu wa mwili - kwa magonjwa, ajali, nk. Uangamivu huu wote una njia ya kupona, lakini kuna aina moja ya uangamivu ambayo ni ya mwisho nayo ni mauti. Mauti ni uangamivu wa kutisha sana!

Huenda nyote mmehudhuria mazishi wakati fulani au katika maisha yenu! Je, unakumbuka hali ya kukataa tamaa kabisa na hisia za kutisha za kufiwa kwenye mazishi yote? Ilikuwa hivyo pia kwenye mazishi ya kwanza ya wanadamu. Funga tu macho na uwazie jinsi mambo yalivyokuwa! Kaini, baada ya kutambua kwamba alikuwa amemfanyia abeli jambo baya na kuona damu kila mahali atakuwa alikimbia na kujificha kutoka kwa wazazi wake, labda na dada zake wadogo. Kadiri muda ulivyopita na watoto hawakurudi nyumbani adamu na eva wakiwa na wasiwasi, wangeenda kutafuta, na baada ya muda wangemgundua abeli akiwa anaonekana kulala huku akivuja damu. Wangejaribu kumuamsha habili kwa kumtingisha taratibu na walipoona hakuna majibu pengine eva angemwambia adamu - "sijawahi kumuona habili akilala usingizi mzito kiasi hiki" na kadri muda ulivyosonga na habili aliendelea kulala na mwili ulianza kubadilika taratibu na kuwa mkakamavu, wazo lingemjia adamu kuwa mwanawe abeli amekufa! Na kwamba hiki ndicho kile ambacho bwana mungu alimaanisha kwa kusema hakika mtakufa!

Na mtu anaweza kufikiria tu matukio ya huzuni na maombolezo ambayo yangetokea kutoka kwa adamu na eva na familia yake ndogo kwenye mazishi yale ya kwanza ya nchi!

Hakika! Hii ndiyo "njia" ya dhambi na mauti iliyoanzia hapo na ambayo ulimwengu wote wa wanadamu sasa unatembea ndani yake! Hii ndiyo njia pana inayopelekea kwenye "njia za mauti" au "uangamivu." Mabilioni mengi duniani wanatembea kwenye njia hii kama tunavyosoma – "*nao ni wengi waingaio humo….*"

Njia hii pana ya dhambi imekuwa hali ya kurithi ambayo mtu anaipokea pale tu anapozaliwa kama tunavyosoma katika zaburi 51:5 "*tazama, mimi naliumbwa katika hali ya uovu; mama yangu alinichukua mimba hatiani*." Wengi hawajaelewa kina cha mstari huu na wanafikiri kwamba mfalme daudi mtunga-zaburi anajisemea yeye tu! Lakini sio hivyo! Maana tunasoma kwa uwazi sana jambo hili hili katika warumi 5:12 "*kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi*." "mauti" na "hali ya dhambi" vilipitishwa kwa wanadamu wote wakati wa kutungwa mimba tumboni mwa mama!

Daudi alitueleza kweli hii kuu kwa uwazi sana! Alikuwa ni adamu "mtu mmoja" ambaye alikuwa wa kwanza "kukata utepe" wa dhambi kisha kuingia na kutembea katika njia hii. Ilimchukua miaka 930 (mwanzo 5:5) kutembea hadi mwisho (uangamivu-mauti) lakini leo safari inakamilika kwa haraka zaidi - miaka 80/miaka 60 au hata miaka 30!

Kwanini iko hivyo? Kwa sababu kwa karibu karne 60 au miaka 6000 na baada ya kutembea kwingi katika 'njia' hiyo, basi imekuwa "laini" (ni rahisi kufanya dhambi) na sasa mtu anaweza "kuteleleza" (kwa silika na moja kwa moja) juu yake na hivyo kufikia mwisho kwa haraka sana. Kwa maana dhambi imekuwa ya kawaida kwa

mwanadamu na kutenda dhambi rahisi zaidi kuliko kutenda haki! Dhambi imeingia ndani ya damu na jeni za mwanadamu. Dhambi imekua kwa kiwango kikubwa kiasi kwamba wanadamu wamepoteza kabisa njia za haki hata imeandikwa katika maandiko katika mithali 14:12 - "*iko njia ionekanayo kuwa ni sawa machoni pa mwanadamu ....*" je, unaweza kufikiria? Leo, njia za dhambi zinaonekana kuwa sahihi na kukubalika machoni pa mwanadamu.

Ili kuelewa vizuri zaidi kina cha ukweli huu, hebu tuchukue mifano michache ya njia za dhambi ambazo sasa zimeenea sana kwa wanadamu -

**1. Uongo**

Hii ni kusema yale ambayo si ya kweli. Inasemekana tunazungumza maneno 250 ya uongo kwa siku! Inaonekana ni jambo la ajabu lakini hebu tuchunguze njia ambazo tunadanganya.

Uongo katika salamu na kujibu salamu rahisi ya "habari yako?" hata kama mtu alikuwa mgonjwa na hana furaha jibu moja kwa moja ni "sijambo"!!

Uongo kwenye biashara na maofisini katika miingiliano kuhusu bei, uwasilishaji na ahadi za wakati, n.k. uongo nyumbani na unapotembelea nyumba zingine kuhusu chakula kinachotolewa na ladha yake! Chakula kinaweza kisimridhishe mtu lakini jibu linalototolewa kwa swali la – “chakula kikoje?” Ni – “wow! Ni kitamu ulipata wapi mapishi? Naweza kuipata?"

Uongo kwa watoto ili kuwafanya watii kwa kuwaongelea viumbe wa kufikirika wa kutisha kama vile "boogeyman", n.k! Kudai uongo kwa mambo marahisi kuwa… uongo “mweupe” na kwamba mungu hapendezwi na uongo “mweusi” tu katika mambo mazito. Tunasema uongo na kusema- "kweli" baada ya hapo! Kwa hivyo, basi kuna

"uongo halisi!" — "uongo wa kweli!" Filamu ya kiingereza ilikuwa na kichwa- "uongo wa kweli!" - hebu fikiria! Uongo na kudanganya umechanganyika sana katika damu ya watu hata wanadanganya kama vile ni kawaida! Kusema ukweli sasa inakuwa ngumu, ngumu sana!!

Hebu na tuchunguze dhambi nyingine -

2. **Usingiziaji/umbea**

Hii ni kuzungumza kuhusu tabia za wengine na matendo yao uwazi wazi na hadharani kupitia majadiliano na mazungumzo na majirani au kupitia magazeti, karamu, n.k inachukuliwa kuwa ni kitu cha "kufurahisha" kujadili maisha ya watu wengine na "udhaifu" na matendo yao. Inaitwa ... "muda kupita" siku zote ni kumhusu mtu mwingine! Msengenyaji/mbea hangetaka maneno yaleyale yasemwa juu yake mwenyewe. Suala hili zito la uchafuzi wa tabia huchukuliwa kirahisi sana na limekuwa jambo la kujipatia raha na hata burudani leo!

Kisha na tuchunguze dhambi nyingine kubwa -

3. Ubinafsi

Hii ni hali ya kujifikiri, na kujiinua "binafsi" katika hali na nyakati zote za maisha ya kila siku. Huonyeshwa katika maisha ya kila siku, katika maeneo kama vile:

Nyumbani na miongoni mwa familia... Kuhusiana na matumizi ya vifaa vya nyumbani na kazi za nyumbani, n.k. katika mabasi na treni na ndege kwa nafasi ya kukaa na matumizi ya vifaa n.k.

Shuleni na miongoni mwa watoto wa shule darasani na katika uwanja wa michezo. Katika biashara, pamoja na shughuli za kila siku na

kufanya kazi mbalimbali….miongoni mwa viongozi na wanasiasa na katika migogoro ya nchi mbalimbali juu ya maji, ardhi n.k.

Sehemu kubwa ya shida na misukosuko yote duniani ina mzizi wake katika ubinafsi. Na orodha ya dhambi inaweza kuendelea zaidi na zaidi…

Hii ndiyo njia pana au "njia" ambayo sasa wengi wa ulimwengu wamekuwa wakisafiri humo na inaelekea kwenye uangamivu au mauti. Hii ndiyo "njia" ya dhambi ambayo yesu alituambia kuihusu *"…. Nao ni wengi wanaoingia humo."*

Kwa hivyo, kwenye chati ya mpango wa kimungu pia tunaona "kuanguka" kutoka kwa usawa "n" hadi usawa "r" kama njia pana. Ulimwengu mzima katika ulimwengu wa kwanza na wa pili unaonyeshwa kama kwenye usawa "r".

Israeli wakati wa enzi ya kiyahudi inaonekana kwenye usawa "p" ambao uko karibu na usawa "n" lakini chini yake……..inawakilisha hali maalum ya israeli kwa vile walipokea kuhesabiwa haki ya mfano kwa njia ya sadaka za kila mwaka za siku ya upatanisho (mambo ya walawi 16:29-30) kisha mungu aliwapa israeli sheria na ilikuwa na ahadi ambayo tunaisoma katika wagalatia 3:12 "*na torati si ya imani; bali mtu azitendaye hayo ataishi katika hayo.*"

Mungu aliwapa israeli sheria kupitia musa kama "njia" ya uzima lakini hakuna yoyote angeweza kuipata kwa kuwa sheria iliyo kamili ya mungu haiweza kushikwa na mwanadamu aliyeanguka na asiyemkamilifu (wagalatia 2:16). Hivyo, waisraeli wote nao walikufa! Hii basi ilikuwa njia pana iendayo kwenye "uangamivu" au mauti na ilikuwa njia pekee iliyokuwa wazi kwa ulimwengu na israel hadi alipokuja yesu. Kutoka kwa adamu hadi kwa yesu njia pekee ya iliyofunguliwa kwa yote ilikuwa njia pana!

**Njia ya pili - njia finyu**

Kwa kifo cha yesu ndipo ilipofunguliwa njia mpya. Hebu tusome kuhusu "njia" hii katika… waebrania 10:19,20 "*basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya yesu, kwa njia mpya, iliyo hai, aliyoiweka kwa ajili yetu, ipitayo katika pazia, yaani, mwili wake*" yesu kupitia kifo chake msalabani alifungua "njia mpya na iliyo hai" njia ya uzima! Na hiyo ndiyo "njia" ambayo yesu alirejelea katika mathayo 7:14 "*kwa maana mlango ni mwembamba, na njia ni finyu iendayo uzimani, nao waionao ni wachache*."

Hii ilikuwa njia mpya, na ilikuwa ni ya "uzima" na yesu alipendekeza kuingia katika njia hiyo tunaposoma kwa uwazi sana katika mathayo 7:13 "*ingieni kwa mlango ulio mwembamba….*"

Hii ina maana gani? Njia hii ni ipi? Na "uzima" huu ni upi?

"kupasuka" kwa pazia katika hekalu la kuingilia patakatifu pa patakatifu wakati wa kifo cha yesu ilikuwa ni ishara ya kufunguliwa kwa njia hii finyu! Tunasoma juu ya jambo hili lililoelezewa katika maandiko haya katika - mathayo 27:51; luka 23:45; marko 15:38 "na tazama, ***pazia la hekalu likapasuka vipande viwili*** toka juu hata chini; nchi ikatetemeka, miamba ikapasuka; "na jua likatiwa giza, na **pazia la hekalu likapasuka katikati.**" " **pazia la hekalu likapasuka vipande viwili** toka juu hata chini." ni ishara gani kubwa ya kufunguliwa kwa njia hii! Pazia la patakatifu pa patakatifu lilikuwa zito na nene sana kiasi kwamba halingeweza hata kuinuliwa na kuhani mkuu alipoingia humo mara moja kwa mwaka! Ilimbidi kutambaa chini yake! Na fikiria pazia nene jinsi hiyo ikichanika yenyewe! Ilikuwa ajabu ya maajabu!

Sasa tuelewe kwanza umuhimu wa kupasuka kwa pazia hili tunaposoma katika waebrania 9:2-8 “*maana hema ilitengenezwa, ile ya kwanza, mlimokuwa na kinara cha taa, na meza, na mikate ya wonyesho; ndipo palipoitwa, patakatifu. Na nyuma ya pazia la pili, ile hema iitwayo patakatifu pa patakatifu, yenye chetezo cha dhahabu, na sanduku la agano lililofunikwa kwa dhahabu pande zote, mlimokuwa na kopo la dhahabu lenye ile mana, na ile fimbo ya haruni iliyochipuka, na vile vibao vya agano; na juu yake makerubi ya utukufu, yakikitia kivuli kiti cha rehema; basi hatuna nafasi sasa ya kueleza habari za vitu hivi kimoja kimoja. Basi, vitu hivi vikiisha kutengenezwa hivyo, makuhani huingia katika hema hiyo ya kwanza daima, wakiyatimiza mambo ya ibada. Lakini katika hema hiyo ya pili kuhani mkuu huingia peke yake, mara moja kila mwaka; wala si pasipo damu, atoayo kwa ajili ya nafsi yake na kwa dhambi za kutokujua za hao watu. Roho mtakatifu akionyesha neno hili, ya kwamba njia ya kupaingia patakatifu ilikuwa haijadhihirishwa bado, hapo hema ya kwanza ilipokuwa ingali ikisimama*”

Hema ya mungu ambayo musa aliagizwa kuijenga (kutoka 25:9) ilikuwa na chumba cha ndani kabisa .... “patakatifu pa patakatifu” na iliwakilisha mbinguni na uwepo wa mungu. Mwanga wa shekina hapo ukiwakilisha uwepo wa mungu mwenyewe!! (maelezo ya habari hii yatachukuliwa katika somo la 31)

Hii ndiyo ndiyo "njia" iliyofunguliwa na yesu ➞ njia inayoelekea mbinguni!!

Ni wokovu ambao tunasoma maelezo yake katika - waebrania 2:3,4 “*tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii; ambao hapo kwanza ulianza kunenwa na bwana, kisha ukathibitishwa kwetu na wale waliosikia; mungu naye akiwashuhudia kwa ishara na maajabu na kwa miujiza ya namna nyingi na karama za roho mtakatifu, kama apendavyo yeye mwenyewe?*”

“njia” hii pia inaitwa “wokovu mkuu namna hii” na ni wokovu wa mbinguni ambao mtume paulo anazungumzia katika wafilipi 3:14. “*nakaza mwendo, niifikilie mede ya thawabu ya mwito mkuu wa mungu katika kristo yesu*.” Na ni nini basi "uzima" huu ambao unafikiwa kwa njia finyu? Tunasoma juu yake ikifafanuliwa katika - warumi 2:7 "*kwa wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokufa...*" “uzima” unaotolewa, tunasoma hapa kuwa ni "kutokufa." hii ina maana gani? Kutokufa ni nini? Wengi hawana uelewa wa wazi wa maana ya kutokufa. Inadhaniwa kwamba wanadamu wote kimsingi hawawezi kufa kwa kuwa nafsi zao haziwezi kufa!

Je, biblia inafundisha hivyo? Hebu tujifunze jambo hilo katika 1timotheo 6:16 “*yeye pekee aliye na kutokufa, akikaa katika nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuikaribia*.” Sasa huyu "ambaye pekee ana kutokufa" ni nani? Hawezi kuwa ni yesu kwani tunasoma hapa – “ambaye hakuna mtu aliyemwona wala awezaye kumwona. Ni baba wa mbinguni! Biblia inatufundisha kwamba yeye “tu” ndiye aliyekuwa na kutokufa hapo mwanzo.

Viumbe wote hai mbinguni na duniani waliumbwa wenye kufa[2]. Mbinguni kulikuwa na viumbe vya roho vyenye kufa wakati adamu alikuwa mwanadamu mwenye kufa. Watu wenye kufa ni viumbe ambao wana uzima ndani yao lakini… wanaweza kufa. Wenye kutokufa ni wale ambao hawawezi kufa kabisa! Kutokufa ni pale ambapo mauti haiwezekani kabisa!

---

[2] *Tunaposema **wenye kufa** haumaanishi kwamba viumbe hao wana hali ya kufa ndani yao bali tunamaanisha kwamba ikitokea sababu ya wao kufa basi wanaweza kufa, na isipotokea sababu basi wataendelea kuishi milele. Walakini kwa habari ya **wenye kutokufa** ni kwamba hata itokee sababu ya kufa, hakuna uwezekano kabisa wa kufa.*

Na vipi kuhusu jamii ya wanadamu? Hebu sasa tusome maneno ya yesu katika luka 9:60 "yesu akamwambia, waache wafu wazike wafu wao." Wana wote wa adamu hata hawaelezwi kuwa wa kufa bali… kama "wafu" kwa sababu baada ya anguko la edeni wote wanazaliwa wakiwa wafu tayari, wakiwa hawana haki ya kuishi hata kabisa! Viumbe hai wenye kufa wana haki ya kuishi - kama malaika mbinguni.

Na vipi kuhusu yesu? Hebu tusome habari zake katika – ufunuo 1:18 "*mimi ndimi niliye hai, nami nilikufa…*" huyu ni yesu anazungumza na anasema nini? "nilikuwa nimekufa". Hata yesu alikufa kama mwanadamu mkamilifu mwenye kufa pale msalabani kama tunavyosoma katika mathayo 27:50- "*yesu akiisha kupaza sauti tena, akatoa roho*".

Lakini baada ya siku ya tatu yesu alipewa kutokufa kwa baba (yohana 5:26 – "*…amempa na mwana….*") Na…. Sasa ni mwenye kutokufa kama tunavyosoma katika ufunuo 1:18 "…na tazama, ni hai hata milele na milele, amina"

Baada ya kuelewa haya sasa na tusome jambo lingine muhimu katika – 2 petro 1:4 "*tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa* ***asili ya uungu****, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kupitia tamaa*." Wafuasi wa yesu sasa wakiwa bado katika enzi/zama hii ya injili wanaahidiwa pia "uzima" huu juu ya asili ya uungu ya kutokufa! Inaonekana kama kitu cha kutosadikika

Lakini tusome na kuthibitisha jambo hilo katika maandiko mengine katika – 1 wakorintho 15:53; "*kwa maana huu uharibikao lazima uvae kutokuharibika, na huu wa kufa uvae kutokufa*." Ufunuo 20:6 "*heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu yao hao*

*mauti ya pili haina nguvu* .” Hapa tena imetajwa hiyo ahadi ya kutokufa katika kile kiitwacho ufufuo wa kwanza,

Ahadi hii ya kutokufa inatajwa pia na mtume paulo kama “taji” katika 2 timotheo 4:8 – “*baada ya hayo nimewekewa* ***taji ya haki****...*” Ni kwa ahadi hii akilini kwamba mtume paulo anawaandikia wakristo katika – “warumi 12:1” *basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai*.”

Tazama! Hapa mtume paulo anawasihi (anawasihi na kuwaomba) “ndugu” (waumini)… “watoe miili yao iwe dhabihu iliyo hai”

Kwa nini? Hii ina maana gani?

Hii inazungumza juu ya maisha ya kujidhabihu… kwa kufuata nyayo za yesu. Tena, tunasoma juu ya jambo hilo hilo kwa uwazi sana katika wafilipi 1:29; na 2timotheo 2:11,12 “maana mmepewa kwa ajili ya kristo, si kumwamini yeye tu, bali na kuteswa kwa ajili yake. Ikiwa tumekufa pamoja naye, tutaishi pia pamoja naye.” "tukiteseka pamoja nae, tutatawala pamoja naye"

Njia ya kikristo si kuamini tu bali pia kumfuata bwana katika dhabihu na kifo, lakini tunasoma kwamba - "nao ni wachache (wakristo) wawe waupatao" (elewa fursa hii kuu na upendeleo)

Yesu mahali pengine alieleza njia hii finyu kwa kauli ambayo wengi hawajaielewa waziwazi, na kwa kweli wengi hata wameelewa vibaya! Maneno haya tunayasoma sasa kutoka katika – mathayo 19:24 “tena nawaambia, ni vyepesi ngamia kupenya tundu la sindano, kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa mungu.” Andiko hili limerudiwa katika - marko 10:25 na luka 18:25

Nini maana yake?

Ikichukuliwa kihalisia ni upuuzi kabisa hata, kuzingatia!

Lakini kuna wakosoaji wa biblia ambao wananukuu mstari huu pamoja na mistari mingine na kuutumia kama mfano kuonyesha kwamba mafundisho ya yesu hayakuwa na msingi na ukweli!

Ni lazima tukumbuke kwamba maneno ya yesu, pamoja na kuwa ya kimafumbo katika asili yake, pia yalikuwa na maeneo na mambo aliyoona kumzunguka na kuyatumia katika mafundisho yake. Huu ni mmoja wa mfano wa namna hiyo! Tutaona mengi zaidi kama hayo katika madarasa yanayokuja!

Yesu alimaanisha nini hapa kwa maneno…. "tundu la sindano"?

Yesu alikuwa anarejelea hapa "lango" ndani ya lango kuu la yerusalemu! Huwa inatokea kwamba milango mikuu ilipofungwa baada ya jua kutua, wafanyabiashara waliokuwa wakirejea walitakiwa kushuka kwenye ngamia zao (magari yao ya usafiri) na kushusha shehena ya bidhaa na mizigo waliyokuwa wamebeba na kisha kumruhusu ngamia kuingia kwa kupinda kwenye lango hilo kisha wabebe bidhaa wenyewe kupitia lango hilo, na hatimaye kupakia tena ngamia kisha waendelee! Hii ilikuwa njia ya kuingia kwa "tundu la shindano" na yesu alikuwa anazungumza juu ya ugumu. Tajiri akifika getini, huenda alidhani haiwezekani (kwa kuwa ana mizigo mingi ya kushusha kisha kupitisha kimoja kimoja mpaka amalize), lakini ijapokuwa ni ngumu, bado ilikuwa inawezekana! Hivyo pia njia finyu katika kumfuata yesu inaonekana kuwa haiwezekani mwanzoni kwa wengi lakini inawezekana kweli, la sivyo mungu asingetoa wito wa namna hii! Tutajifunza maelezo zaidi kuhusu wito huu maalum wa kikristo na "namna ya maisha" katika madarasa yajayo (katika darasa #17, 18, & 19). Kwa hiyo ndugu wapendwa hii ndiyo njia finyu ya kuelekea utukufu mkubwa!

Sasa, tuje kwenye njia ya tatu! Je, kweli kuna njia ya tatu? Njia hii ni ipi?

Tuliona kwamba kwa njia pana ulimwengu wote waliotembea ndani yake- njia ya dhambi- walikuwa wamekwenda kwenye "uangamivu" au mauti.

Je huo ndio mwisho kwa wanadamu wote? Je, hakuna tumaini kwa wanadamu wote ambao… hawajawahi kusikia habari za yesu au …hawajawahi kumwamini? Je, yesu siyo mwokozi wa ulimwengu pia?

Hebu tusome jibu hilo kwa uwazi kabisa katika 1 yohana 2:2 "*naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu wote*." Ndiyo! Kifo cha yesu juu ya msalaba wa kalvari haikuwa tu kwa ajili ya "zetu" - dhambi za kanisa bali. Pia, kwa dhambi za ulimwengu wote!

Na hili tunalisoma tena kwa uwazi kabisa katika 1timotheo 2:6 "…. *Ambaye alijitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote kushuhudiwa kwa wakati wake.*" Yesu alitoa uhai wake kuwa bei ya kuondolewa kutoka katika mauti kwa wote! Kwa hivyo, lazima tutarajie ulimwengu pia kuwa na……. Wokovu!

Wokovu wa ulimwengu ndio njia **ya tatu** ambayo tunaenda kutambulishwa na kuona sasa!

**Njia ya tatu – njia kuu**

Huo wokovu wa ulimwengu utakuaje? Tusome juu yake katika isaya 35:8 "*na hapo patakuwa na njia kuu, na njia, nayo itaitwa, njia ya utakatifu; bali **itakuwa kwa hao, wasafirio**, wajapokuwa wajinga, hawatapotea katika njia hiyo …*"

Ni kwa ajili ya "wasafiri." Hii inarejelea wenye dhambi! Ulimwengu wa wanadamu bila msaada chini ya ushawishi wa dhambi. Lakini ni

nani wanamaanishwa kama "wajinga"? Hebu tuone katika maandiko tunaposoma kutoka - zaburi 14:1 "*mpumbavu(mjinga) amesema moyoni, hakuna mungu…*" "wajinga" ni wasomi na wanasayansi wakubwa wa ulimwengu! Wale ambao sasa wanatangaza kwa uwazi kwamba ulimwengu hauna muumba binafsi na…… kwamba hakuna anayeitwa mungu bali kwamba viumbe vyote vilifanyika na kuwapo kwa sababu ya hali fulani huko nyuma.

Hakika, hawa ndio "wajinga" ambao hawatadanganyika katika njia kuu, hawataweza tena kujikwaa katika uelewa wao kwa sababu tunasoma kuwahusu katika isaya 29:24 "*hao nao waliokosa katika roho watapata ufahamu, na hao wanung'unikao watapokea mafundisho.*"

Sasa na tuone zaidi kuhusu njia hii katika isaya 35:9 "hapatakuwa na simba huko……."

Je, hii inamrejea simba mnyama? Hakutakuwa na simba tena basi? Hilo litahuzunisha kama nini! Kwa sababu simba ni mnyama mzuri na wa kushangaza! Naye ndiye… mfalme wa nyika!

Ni wangapi wanaokimbilia kwenye mbuga ya wanyama ili kumtazama simba tu! Je, hii basi ni kauli halisi?

Hapana! Simba anayerejelewa hapa ni "simba" ambaye tunasoma habari zake katika 1 petro 5:8 "*kwa sababu mshitaki wenu ibilisi kama simba angurumaye…*" ndiyo! Ni shetani anayerejelewa hapa kama……"simba." Andiko hili linarejelea ukweli kwamba atakuwa… amefungwa katika kipindi hicho ili asiweze kuwadanganya watu kama tunavyosoma katika ufunuo 20:3-"*akamtupa katika kuzimu, akamfunga, akatia muhuri juu yake, asipate kuwadanganya mataifa tena...*"

Tazama! Shetani "simba" atafungwa na hataruhusiwa kuwadanganya watu. Kisha tunasoma nini tunapoendelea katika - isaya 35:9,10 "…. *Hapana mnyama mkali atakayepanda juu yake…*"

Hii inamaanisha nini? Tuliona kwamba “simba” anafananisha shetani-hivyo pia hawa “wanyama wakali” lazima wafananishe kitu fulani cha shetani na… chini ya udhibiti wa shetani kama ambavyo hata simba ni mfalme wa hayawani wote.

Hiwa wanarejelea mifumo yote ya shetani na vyanzo vya uovu - baa, pango za kamari, ukahaba, sinema na tv za kupotosha, n.k. haya yote yanaongoza kwenye njia za dhambi na polepole huleta uangamivu (mauti).

Tunasoma nini juu ya hawa wanyama wakali? “…. Hawatakuwepo humo…” ndiyo! Katika njia hiyo, vyanzo vyote hivi vya dhambi na majaribu havitakuwepo tena!! Kutakuwa na mfumo mpya wa ulimwengu!

Hebu tuendelee kusoma kutoka katika andiko hilo katika isaya 35:9 *“… bali waliokombolewa watakwenda katika njia hiyo. Na hao waliokombolewa na bwana watarudi,…”*

Hapa tunasoma “waliokombolewa na bwana” wakirudi! Hii ina maana gani?

Ah, ndio! “waliokombolewa na bwana” hapa wanarejelea ulimwengu wa wanadamu ambao ndipo watarudi kutoka “walipokwenda”

Ulimwengu wote ulienda wapi? Tulisoma hapo awali kwamba ulimwengu wote unatembea katika njia pana iendayo kwenye “uangamivu” ambao ni mauti, lakini sasa kwa neema ya dhabihu ya fidia ya yesu watarudi kwa “kufufuka kwa wafu” (danieli 12:2).

Kwa maana tunasoma kwamba huo utakuwa wakati ambapo wote watafanywa hai tena kama tunavyosoma kwa ufasaha sana katika – 1 wakorintho 15:22 “…*kadhalika katika kristo wote watahuishwa*…” hivyo, wote watafufuliwa kama mtume paulo anavyolithibitisha jambo hilo

na kutuambia katika matendo 24:15 “*ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia*”

Hili linathibitishwa tunaposoma mapenzi ya mungu kwa wanadamu pia katika 1 timotheo 2:3, 4 “*...ambaye hutaka watu wote waokolewe na kupata ujuzi wa kweli.*” Haya ni mapenzi ya mungu! Na hakika itatimia. Siku hiyo tukufu na ya ajabu haiko mbali sana!

Sasa "kuokolewa" inamaanisha nini?

Ikiwa itaeleweka kwa usahihi katika lugha ya kibiblia inarejelea kuokolewa kutoka kwa mauti! Mstari huu unarejelea hatua mbili za wokovu wa wanadamu. Kwanza… ukombozi kutoka kwa mauti na kisha pili wale walioamshwa lazima wakombolewe kutoka katika hali yake ya dhambi.

Hivyo “wote” wataokolewa kutoka kwa mauti kwa njia ya ufufuo kwa wote na kisha “watakuja kwenye ujuzi wa kweli”

Maajabu haya makuu ya ufufuo yatatokeaje?

Hebu tusome kutoka katika maandiko sasa katika – luka 13:29,30 “*nao watakuja kutoka mashariki na kutoka magharibi na kutoka kaskazini na kutoka kusini, nao wataketi katika ufalme wa mungu. Na tazama, wako wa mwisho watakaokuwa wa kwanza, na wako wa kwanza watakaokuwa wa mwisho.*”

Hii hapa ndo siri ya namna ufufuo wa wafu utafanyika!! “…. Wako wa mwisho (kufa) watakaokuwa wa kwanza (kufufuka katika wafu). …… na wako wa kwanza (kufa) watakaokuwa wa mwisho (kufufuka katika wafu)

Hakika! Lazima kuwepo na utaratibu! Kizazi cha mwisho kitakachokufa, wakati wa ufufuo kitakuwa cha kwanza kuinuka…wakati kizazi cha kwanza kufa (adamu na kizazi chake)

watakuwa………. Wa mwisho kuinuka!! Sasa hii ni kuruhusu kubadilishwa na kurekebishwa kwa hali ya ufalme kwa zile familia zinazojuana, jamaa na marafiki. Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu hali ya mtu na mwili yake itakuwa sawa na ilivyokuwa wakati wa kufa…. Kiakili na kimwili! Hakutakuwa na mabadiliko kabisa!

Hili lipata kuthibitishwa kwetu katika maandiko katika ayubu 19:26,27 *"na ijapokuwa wadudu wa ngozi yangu watauharibu mwili huu, lakini katika mwili wangu nitamwona mungu.* ***Nitamwona mimi mwenyewe, na macho yangu yatamwona, wala si mwingine****…"*

Tafadhali zingatia maneno - "nitamwona mimi mwenyewe, na macho yangu yatamwona, wala si mwingine;" ndiyo! Hakutakuwa na mabadiliko katika utu kabisa! Kila mmoja ataweza kujitambua kwa asili bila mabadiliko yoyote! Hivyo basi, kinachofuata lazima uje ukombozi kutoka katika hali ya dhambi!

Hilo litatimizwaje? Tunasoma jibu katika yohana 17:17 *"….uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli."*

Utakaso kutoka katika njia za dhambi unawezekana tu kwa nguvu ya kweli! Kwa hivyo wote "…. Lazima wafikie ujuzi wa kweli" ili kupata kutakaswa kutoka katika njia za dhambi.

Je, hili litafanywaje?

Hatua ya kwanza itakuwa kama tunavyosoma katika isaya 29:18; 32:3 *"na siku hiyo viziwi watasikia maneno ya kitabu, na macho ya vipofu yataona katika utusitusi wa giza. "na macho yao waonao hayatafifia, na masikio yao wasikiao yatasikiliza.*[3]"

---

[3] *Neno la kiebrania lililotafsiriwa "yatasikiliza" lina maana ya kuzingatia, kutilia maanani, kuangalia kwa jicho la uelewa (ufahamu), kutii.*

Hakika hii hairejelei macho na masikio halisi! Hii inatufundisha jinsi "macho" na "masikio" yote ya ufahamu ya ulimwengu yatavyofumbuliwa kutoka kwenye athari za upofushaji za shetani!

Ulimwengu wote utaachiliwa kutoka katika upofu huu ili kuelewa mafundisho ya uongo, ushirikina, n.k ….na kutambua kweli ya biblia ya mungu ambayoo hapo awali hawakuweza kuuona(kutambua) kwa sababu tunayoisoma katika - 2 wakorintho 4:4 ". *...mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini….*" Shetani alikuwa amepofusha akili zao kwa… udanganyifu na uongo!

Kisha tunasoma juu ya kusambaa kwa kweli katika -. Habakuki 2:14 "*kwa maana dunia itajawa na maarifa ya utukufu wa bwana….*" Neno - kweli itatawanywa ulimwenguni kote.

Unaweza kujiuliza, ni kivipi?

Kwa vyombo vya habari ambavyo tunaviona mbele ya macho yetu leo - tv, redio, sinema, vitabu, intaneti, kompyuta n.k.

Hivyo, hii njia kuu inaitwa- "njia ya utakatifu" - -……njia ya kufikia ukamilifu!!

Hivyo, taratibu hali ya mauti na ujinga itakuwa imeondolewa kabisa kwa watu wote !!

Haya ndiyo hasa tunayoyaona na kuyasoma katika isaya 25:7 "*naye katika mlima huu atauharibu uso wa **sitara** uliowekwa juu ya watu wote, na **utaji** ule uliotandwa juu ya mataifa yote*."

Hii ina maana gani? Hizi ni ishara na zinaashiria:–

"**sitara**" hii inaashiria kifo cha kurithi cha adamu kinachofunika juu ya mwanadamu wote. Kama tunavyosoma: "kama vile katika adamu wote hufa…" na kisha tunasoma juu ya – "utaji" hii inaashiria

kufungwa kwa macho ya ufahamu kwa wanadamu wote tunaposoma katika – isaya 60:2 "*kwa maana, tazama, giza litaifunika dunia, na giza kuu litaifunika kabila za watu; …*" Na pia, 2 wakorintho 4:4 "*ambao ndani yao mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie nuru ya injili ya utukufu wake kristo aliye sura yake mungu*."

Na kutakuwa na vichocheo vingi vya utii katika hii njia kuu kama tunavyosoma kutoka katika – ayubu 33:24, 25 "*nyama yake itakuwa laini kuliko ya mtoto atazirudia siku za ujana wake*." Mstari huu unazungumza juu ya jambo la ajabu sana…. Kitu kisichowaziwa kabisa na mwanadamu! Watu, siku baada ya siku watatoka katika hali ya uzee hadi kuwa vijana! Mvi zitageuka kuwa nyeusi! Ngozi iliyokunjamana itakuwa laini! Udhaifu utabadilika na kuwa nguvu! Meno yaliyoanguka yataanza kurudi! Mapungufu yote yatatoweka polepole kadri ukamilifu unavyoonekana!

Halafu kutakuwa na kipindi cha hukumu cha ukarimu sana! Hili tunasoma katika isaya 65:20 "*kwa maana mtoto atakufa mwenye umri wa miaka mia; bali mtenda dhambi mwenye umri wa miaka mia atalaaniwa*."

Wote wanapaswa kupokea kipindi cha hukumu cha miaka 100 ya kupata nafasi ya toba na matengenezo kutoka katika njia za dhambi. Fikiria tu! Leo maisha yenyewe hayagusi kiasi hicho cha miaka!! Ni kipindi kirefu cha neema kilichoje mungu ametenga kuwahimiza wanadamu wote kutubu kutoka katika njia za dhambi! Ah! Je, kutakuwa na watu wasiotii kwa makusudi wakati huo? Tunasoma juu ya jibu hilo pia katika maandiko katika isaya 26:10 "*mtu mbaya ajapofadhiliwa, hata hivyo hatajifunza haki; katika nchi ya unyofu atatenda udhalimu…*"

Kutakuwa na wengine licha ya neema na rehema za mungu! Hawa watachagua kutotubu au kuzirekebisha njia zao za dhambi.

Watachukua njia ya shetani kwa maana ya kuwa maadui wa mungu na… wa haki.

Lakini je, tunasoma nini kuhusu wengine?

hebu tusome sasa kutoka katika isaya 35:10 "*…watafika sayuni wakiimba; na furaha ya milele itakuwa juu ya vichwa vyao; nao watapata kicheko na furaha, huzuni na kuugua zitakimbia*." Na tena, katika zaburi 22:27,28 "*miisho yote ya dunia itakumbuka na kumgeukia bwana; kwa maana ufalme ni wa bwana…*"

Wote (wengi wao) watamgeukia bwana na watatii na kumwabudu!

Je, hii njia ya tatu - njia kuu itafunguliwa lini?


Tunasoma jibu katika 1 wakorintho 15:23 "… *baadaye walio wake kristo, atakapokuja*." Ujio wa pili wa kristo ni…. Ili kufungua hii njia kuu!!

Yesu, bwana wetu hakuzungumzia njia hii katika ujio wake wa mara ya kwanza kwa sababu alikuwa amekuja kufungua…. Njia ya pili - njia finyu iendayo kwenye wokovu mkuu wa mbinguni., .... Lakini katika ujio wake wa mara ya pili atakuja kuifungua hii njia ya tatu - njia kuu.

Njia ya wokovu wa wanadamu wote kurudi kwenye ukamilifu wa kibinadamu ambao mungu alimuumba adamu hapo kwanza. Tumeongozwa kuielewa njia hii ya tatu kutoka katika maandiko leo kwa neema ya roho mtakatifu kwani sasa tuko karibu sana na ufunguzi wa njia hii!

Na hizo ndugu wapendwa zilikuwa "njia tatu" za biblia!!

-amina-



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com  au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***